OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI

SHULE YA SEKONDARI MAMIRE

S.L.P 329,

BABATI,

22/3/2022

MOBILE NO. 0782745937/0759596236

Kumb:Na. MSS/KD.5 /VOL. I/01

JINA LA MWANAFUNZI_____

S.L.P…….

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika Shule ya Sekondari MAMIRE, kwa TAHASUSI ya ..... Uchaguzi huu umezingatia ufaulu wa mwanao katika mitihani ya kidato cha nne iliyofanyika mwaka jana. Hivyo ninatumia fursa hii kukupongeza wewe pamoja na mwanao kwa kupata nafasi hii muhimu. Hongera sana! Karibu sana, Shule ya Sekondari MAMIRE.

MAHALI SHULE ILIPO: Shule ya Sekondari MAMIRE ipo katika Mkoa wa MANYARA Wilaya ya BABATI. Shule ipo umbali kilometa sita (16) toka Babati mjini.

USAFIRI: Upo usafiri mzuri toka Babati kwenda MAMIRE, wakati wote . Nauli :- Babati hadi MAMIRE, Ths.1,000/= kwa HAISI, BAJAJI toka Babati mjini ni Tsh. 8,000/= Bodaboda Tsh. 7000/=

Cha kuzingatia sana ni mwanao awahi shuleni kabla ya saa 11.00 jioni, na si zaidi ya hapo.

SIKU YA KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa tarehe ---------- na siku inayofuata masomo yanaanza rasmi bila kupoteza muda.

Pamoja na barua hii naambatanisha fomu mbalimbali ambazo ni lazima zijazwe vizuri na wahusika na kurudishwa kwa Mkuu wa Shule. Pia utaratibu mzima wa kujiunga na shule umeambatanishwa; tafadhali zingatia sana utaratibu huu na kuutimiza ipasavyo. Ahsante

.....

AKYOO F. MATHAYO

MKUU WA SHULE

Nakala:

1. Afisa Elimu (M), S.L.P. 310, BABATI- MANYARA.

2. Afisa Elimu (W) Sekondari, S.L.P.400, Babati.

3. M/kiti wa Bodi ya Shule, MAMIRE Sekondari, Kumb.Na.MSS/K.5/Vol.I/01

UFUATAO NI UTARATIBU WA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAMIRE.

1. (a) ADA NA MICHANGO YA SHULE KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO ANAYEJIUNGA NA MAMIRE SEKONDARI - KWA MARA YA KWANZA.

Ili kumwezesha mwanao kuishi, na kusoma vizuri katika shule hii ni muhimu sana mzazi/mlezi umlipie mwanao michango kama ifuatavyo, bila usumbufu:

S/N	AINA YA MICHANGO	KIASI	MUDA
1	Ada	70000/=	Kwa mwaka
2	Ukarabati wa samani za shule	10,000/=	Kwa mwaka
3	Maji	5,000/=	Kwa mwaka
4	Taaluma	20,000/=	Kwa mwaka
5	Wahudumu/watumishi wa muda	40,000/=	Kwa mwaka
6	Tahadhari	5,000/=	Mara moja
7	Picha, Kitambulisho na Nembo	8,000/=	Kwa mwaka
8	Huduma ya kwanza	5,000/=	Kwa muhula
9	Bima ya Afya kwa wale wasio na Bima	6,000/=	Kwa mwaka
10	Mitihani	14,000/=	Kwa muhula
11	Michezo	5,000/=	Kwa mwaka
JUMLA 188,000/=			

ANGALIZO: UNASHAURIWA MWANAO AWE NA BIMA YA AFYA

UTARATIBU WA ULIPAJI

1. ADA YA SHULE 70,000/= AC/NO: 40701200105 -Jina Reccurent akaunti Mamire Sec. School.

2. MAJI NA UKARABATI 15,000/= AC/NO: 40710003719 - Jina Self reliance Mamire Sec. School

3. MICHANGO MINGINE 95,000/= AC/NO: 40710003719- Jina Self reliance Mamire Sec. School

4 Nembo na picha 8,000/= Aje nayo mkononi/taslim

AKAUNTI karatasi/risiti ya Benki wakati wa malipo. Aje na Pay in slip tatu tu. Kama inavyoonesha hapo chini.

a) Ada = 70,000/=

b) Ukarabati na Maji 15,000/=

c) Michango mingine 95,000/=

1. b) Mahitaji mengine ambayo lazima mwanao aje nayo ni:-

i) Ream nne (4) ya karatasi A4

ii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia AU 30,000/= aweke kwenye akaunti **40710003719** -JINA LA AKAUNTI SELF RELIANCE MAMIRE SEKONDARI kama ilivyoelekezwa hapo juu.

2**. a) VIFAA VINGINE MUHIMU AMBAVYO LAZIMA AJE NAVYO:**

1. Madaftari yasiyopungua 10 (Counter books) na kalamu za kutosha. (blue /black)

2. Mathematical set – kwa wanafunzi wa sayansi

3. Scientific calculators – kwa wanafunzi wa sayansi na Hisabati.

4. Vifaa vya EK na usafi:- Reki, jembe, rubber squizer hard and soft brush Aje navyo.

5. VYETI: Mwanao aje na:-

- Result slip original ya kidato cha nne.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

LIKIZO: Ni lazima mwanao aende likizo hasa wakati wa likizo ndefu ya June na December.

SIMU: Simu ya mkononi ni marufuku mwanafunzi kumiliki akiwa shuleni, atakapopatikana na kosa hilo atarudishwa nyumbani mara moja na faini ya kiasi cha shilingi 260,000/-. Shule inautaratibu mzuri wa mawasiliano pindi yanapohitajika.

6. MWANAO AJE NA: SARE ZA SHULE, NGUO ZA MICHEZO MATANDIKO NA MAVAZI MENGINE YA KUSHINDIA SHULENI KAMA IFUATAVYO:-

1. Suruali (WAV)/ Sketi (WAS) 2 rangi ya kijivu isiyobana na yenye urefu wa kutosha na upana wa miguuni usiopungua inchi 17 na rinda mbili(suruali), sketi mshono wa V- MBELE urefu kuvuka magoti na Zaidi na ushungi mweupe na nusu kanzu yenye mshono wa solo isiyo na mpasuo kwa wasichana wa kiislamu.

2. Shati 2 nyeupe mikono mirefu

3. Sweta kijivu shingo V isiyo na alama yeyote.

4. Tai kijivu

5. Suruali 1 nyeusi ya kushindia (shamba dress)

6. Wasichana GAUNI rangi LIGHT BLUE mshono wa solo na ushungi mweusi kwa WAISLAMU ya kushindia (shamba dress).

7. Viatu vyeusi vya rangi, visiwe na visigino virefu vya kufunga na kamba

8. Soksi jozi 2 kaki kwa Wavulana na nyeupe kwa wasichana (stocking)

9. Mashuka mawili PINK

10. Michezo: kwa wanafunzi wa sayansi jezi ya dark blue na wanafunzi wa Sanaa jezi nyekundu na viatu vya michezo kwa wote.

11. Truck suit ya BLUE/BLACK BLUE

12. Godoro ft 2½ kwa inchi 3.

13. Mto, Neti, foronya, blanketi na ndoo 1 yenye ujazo wa lita 20

14. Vyombo vya kulia chakula: Sahani, bakuli, kijiko na kikombe, pia unaweza kupata kwenye duka la shule kwa bei ya kawaida.

15. T.shirt yenye nembo ya shule inapatikana Shuleni – kwa Tsh.12, 000/=

Kumb.MSS.Na.K.5/Vol.I/01

SHERIA ZA SHULE

Zipo sheria za shule ambazo ni lazima mwanao azifuate wakati wote atakapokuwa shuleni, kinyume na hapo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu ,Sayansi na Teknolojia ,yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji ELIMU. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuriport shuleni.

i.Heshima kwa viongozi ,wazazi ,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima siku 97 kwa muhula mmoja ahudhurie .

iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

iv.Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazo pangiwa

v.Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa shughuli zote za /safari za kishule

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

ix.Kutunza mali za shule

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi

b) Uasherati na ushoga

c) Ubakaji

d) Ulevi namatumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi ,cocaine ,mirungi, kuberi na kadhalika .

e) Kupiga au kupigana

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

g) Kudharau bendera ya Taifa na alama nyinginezo za Taifa

h) Kuwa mjamzito /kupata mimba au kusababisha mimba kwa mwanafunzi mwenzako

i) Kuoa au kuolewa

j) Kuwa na simu ya mkononi

k) Kutoa mimba

l) Kugoma ,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

m) Kukataa adhabu kwa makusudi

n) Utoro ulio kidhiri zaidi ya siku 90.

Sheria hizi atazikuta shuleni na kusaini fomu maalumu ya kukubali au kukataa kufuata sheria hizo ikiwa ni pamoja na sharia za kuishi Bweni. Endapo atasaini kukataa kuzifuata basi mwanao atarudi nyumbani.

SHERIA /MASHARTI YA KITAALUMA

WITO WETU "NIDHAMU KAZI NA ELIMU"

Jumuiya ya Shule ya Sekondari MAMIRE, inaendelea kuboresha utoaji wa taaluma bora. Kwa maana hiyo basi, mwanafunzi anatakiwa awe na bidii ili kufikia malengo yake, ya mzazi na ya Taifa kwa ujumla. Ili kutilia mkazo katika eneo hili, Bodi ya shule imeamua yafuatayo:

1. Baada ya masomo kuanza kutakuwa na mazoezi mbalimbali ambapo mwanafunzi atapaswa kupata alama si chini ya 60% katika wastani wa masomo yake yote.

2. Endapo atashindwa kupata 60% mara tatu mfululizo bila sababu za msingi, hatua mbalimbali zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kumuita mzazi/mlezi shuleni ili kushauriana kuhusu maendeleo ya mwanae. Ni mategemeo yetu kuwa mwanao atakubali kufuata sheria za shule ili atimize malengo yake ya kitaaluma.

MWANAO AZINGATIE KAULI HII: “KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAMIRE NI HIARI, LAKINI KUFUATA TARATIBU NA KANUNI ZAKE NI LAZIMA ILI KUFIKIA LENGO LILILOKUSUDIWA LA KUTOA ELIMU BORA”. KARIBU SANA MAMIRE SEKONDARI.

.....

AKYOO F. MATHAYO

MKUU WA SHULE

KUPIMA AFYA

Mwanafunzi……..Andika ndiyo katika nafasi mbele ya ugonjwa ambao ulikwishaugua au unaugua:

1.Kifua kikuu……..…..

2.Ugonjwa wa moyo……..

3.Ugojwa wa figo…….

4.Ugonjwa wa akili……..

5.Ajali kubwa……

6.Pumu…….….

7.Vidonda vya tumbo……..….

8.Kifafa…….……

9.Kupasuliwa……

10.Ulemavu……..

KWA MATUMIZI YA KIOFISI TU MGANGA MKUU WILAYA/MKOA

……..…… …… Tafadhali mpime mtajwa kama afya yake inamruhusu aendelee na masomo ya Sekondari kidato cha TANO. Pamoja na haya zingatia maelezo ya mwanafunzi hapo juu. MAELEZO YA MGANGA

…… …… ……

JINA LA MGANGA …… SAINI NA MUHURI…… CHEO…… TAREHE……

Kumb:Na.MSS/K.5/VOL.I/01

TAARIFA JUU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

1. Jina kamili……..

2. Umri……

3. Kazi……

4. Anuani ya nyumbani, namba ya simu za Mzazi/Mlezi……..……..

5. Kijiji……Wilaya……..
Kata……..Mkoa……..…….……..……
Tarafa……..Uraia…….……..

6. (a)Dini ya mzazi/mlezi…….

(b)Namba ya simu (kama ipo)…….Mji…….

7. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe…….

8. Anwani kamali ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo……

9. Anwani ya kazini ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu kila inapobadilika utuarifu rasmi kwa barua kupitia kwa mkuu wa kituo au mwenyekiti wa kijiji chako.

10. Nathibitisha kwamba habari zitolewazo hapo juu ni kamili na kweli Jina la mzazi/mlezi……Saini……Tarahe……

Ninaahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na walimu katika kumlea kijana wangu awe na tabia nzuri siku zote, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo. Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule.Juu ya hayo naelewa kuwa mwanangu akienda kinyume na kifungu cha sheria za shule, hatua za kinidhamu zitafuata ikiwemo kufukuzwa shule. Jina la mzazi/mlezi……Saini……Tarehe……